ISSN 2820-2686 | Toleo la Nane | Julai - Septemba, 2023

# JARIDA LA WAKILI MKUU



**Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana**
Waziri wa Katiba na Sheria

**Dkt. Boniphace N. Luhende**
Wakili Mkuu wa Serikali

## *Karibu Waziri*

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

Sarah Duncan Mwaipopo

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

Prisca Jackson Ulomi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

Prisca Jackson Ulomi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Dennis Julius Buyekwa

Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

Nyamhoni Robert Chacha

Afisa TEHAMA

## Wajumbe

George Nathaniel Mandepo

Mkurugenzi wa Usuluhishi

Hangi Matekeleza Chang'a

Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

Kiuye Mbwana Shemakame

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

CPA Devota Mathew Ngulugulu

Mhasibu Mkuu

Mercy Rowland Kyamba

Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

Zuhura Mohamed Kussaga

Mchumi

# TAHARIRI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) ineendelea kuwa kitovu cha kuandaa viongozi wa Serikali hatua ambayo imesaidia Ofisi kuendelea kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuteua viongozi na kuwakasimu majukumu ya kuendesha baadhi ya taasisi za Serikali na Mahakama ambazo ni nguzo muhimu za utoaji haki nchini.

Katika kudhihirisha hilo, tarehe 3 Septemba 2023, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya uteuzi wa viongozi mbalimbali kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania kwa lengo la kuuongezea nguvu mhimili huo muhimu wenye dhamana ya kutoa haki sawa na kwa wakati kwa wananchi.

Pamoja na viongozi walioteuliwa jicho la Mhe. Rais Dkt. Samia liliiona tena Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kumteua Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

Mafanikio haya makubwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na uongozi thabiti wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambao umekuwa ukisimamia majukumu ya Ofisi ambayo ni kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa weledi na uthabiti wa hali ya juu kwa kufuata Sheria, Taratibu na Kanuni za utumishi wa umma.

Kuteuliwa na kuaminiwa kwa viongozi kutoka OWMS kushika nyadhifa hizo muhimu ndani ya nchi ni ishara njema kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa imeweza kuwaandaa na kuwajenga watumishi wa OWMS kutekeleza majukumu yao waliyokasimiwa kwa manufaa na maslahi mapana ya Taifa.

Katika kuhakikisha Tanzania inakuwa na viongozi mahiri katika Sekta ya Sheria na sekta zisizo za kisheria, Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuwaandaa watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya uongozi ili kukuza ujuzi na ubobezi katika masuala ya uongozi ili waweze kuwa na uelewa mpana katika uongozi ili waweze kumsaidia Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuhakikisha mashauri ya Serikali yanasimamiwa vyema kwa ufanisi na weledi na kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla ili kuendelea kuleta mafanikio makubwa zaidi na kuchangia katika ujenzi wa taifa letu na Ofisi itaendelea kuandaa viongozi mahiri watakaosimamia masuala mbalimbali katika kuhakikisha Serikali inawaletea wananchi wake maendeleo.



**Prisca Jackson Ulomi**
**Mhariri Mkuu**

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



**Sarah D. Mwaipopo**
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Toleo la Nane la Jarida la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni maalum kwa ajili ya kuhabarisha umma kuhusu mambo mbalimbali yaliyojiri katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kipindi kinacho anzia mwezi Julai hadi Septemba Mwaka 2023.

Katika kipindi hicho Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa kuendelea kusimamia vizuri mashauri yote ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na Serikali au dhidi yake hatua ambayo imesaidia kuokoa fedha nyingi ambazo zingelipwa kama Serikali ingeshindwa mashauri hayo Mahakamani.

Kwa kuzingatia majukumu ya Ofisi hii, Toleo la Nane la Jarida ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali litajumuisha matukio yote muhimu yaliyofanyika katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba mwaka 2023 ikihusisha ziara ya Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb) alipoitembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kujionea namna Ofisi hii inavyotekeleza majukumu yake ya kila siku.

Pia, Toleo hili litaendelea kuangazia kwa kina nafasi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kukuza uchumi wa nchi yetu, kuwajengea watumishi na wajumbe wa Menejimenti uwezo kupitia mafunzo mbalimbali yaliyotolewa kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na maelekezo na miongozo iliyotolewa na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Pindi Chana (Mb) alipotembelea Ofisi hii.

Aidha, Toleo hili pia litaangazia uteuzi wa viongozi walioteuliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nyadhifa mbalimbali ikiwemo uteuzi wa aliyekuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

Uteuzi huu unaonyesha namna Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilivyo na uwezo wa kuandaa watumishi wake kuwa viongozi hii inatokana na mshikamano uliopo miongoni mwa watumishi wa OWMS hususani ushirikiano madhubuti uliopo kati ya Menejimenti na watumishi katika kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kufuata misingi, sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma.

Baada ya kuelezea masuala yatakayoakisiwa ndani ya Jarida hili, naomba niendelee kuwasihi wasomaji wetu kuendelea kutoa maoni kwa Bodi ya Uhariri kwa ajili ya kuboresha Jarida hili ili kwa pamoja tuweze kulifanya Jarida hili kuendelea kutoa mchango chanya kupitia matoleo yajayo katika ukuaji wa Sekta ya Sheria hapa nchini. Nawatakia usomaji mwema wa Toleo la Nane la Jarida la Wakili Mkuu.

Ahsanteni.

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. 06 | Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb)Aipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Kulinda Maslahi ya Serikali Ndani na Nje ya Nchi |
| UK. 10 | Rais Dkt. Samia: Ongezeni Tija na Ubunifu katika Shughuli za Kilimo |
| UK. 16 | Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria Kuleta Usawa Nchini |
| UK. 20 | Waziri Mkuu Kassim Majaliwa afungua Maonyesho ya Sabasaba |
| UK. 26 | Jaji Mkuu Ataka Mawakili Kubadilika Kifikra |
| UK. 31 | Mawakili wa Serikali Washirikishwe Kikamilifu katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Kuzuia Migogoro |
| UK. 34 | Mwaipopo: Tekelezeni Majukumu Yenu kwa Kufuata Miongozo Iliyowekwa na Serikali |
| UK. 42 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Kwenye Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria Mkoani Ruvuma |
| UK. 45 | Uteuzi na Taarifa kwa Vyombo vya Habari |
| UK. 50 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yapatiwa Mafunzo ya Udhibiti Ubora |

# *Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) Aipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Kulinda Maslahi ya Serikali Ndani na Nje ya Nchi*



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akizungumza na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipotembelea Ofisi hiyo akiwa kwenye ziara yake ya kikazi Jijini Dar es Salaam.*

Tarehe 13 Septemba 2023, Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), alifanya ziara yake kwa mara ya kwanza ya kutembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) iliyopo jijini Dar es Salaam tangu alipoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongoza Wizara hiyo.

Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amesema kuwa lengo la ziara yake ya kutembelea OWMS ni kufahamu majukumu yao na kujenga uelewa kuhusu namna wanavyotekeleza majukumu hayo ili taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ziweze kushirikiana kuhudumia wananchi kwa kuhakikisha nchi inazingatia misingi ya haki na utawala bora ili taifa la Tanzania liendelee kuwa taifa la amani.

Pia, ameipongeza OWMS kwa kulinda haki na maslahi ya Serikali yasipokonywe ndani na nje ya nchi kwa kushinda kesi ambazo Serikali ilikuwa na haki na kuwa mabingwa katika kutetea vyema Serikali.

“Vile mnavyoitetea Serikali na kushinda kwenye kesi zile ambazo Serikali ilikuwa na

haki, zile fedha mnazoziokoa ndiyo zinasaidia kuleta maendeleo ambapo tunajenga barabara, vituo vya afya. Wakili Mkuu wa Serikali anatetea na kulinda maslahi ya Serikali na taasisi zake tofauti na Mawakili wengine wanaotetea na kulinda maslahi ya taasisi au ya mtu mmoja mmoja," alisisitiza Balozi Dkt. Pindi Chana.

Vile vile amesema kuwa ni muhimu kuwaeleza watanzania utaratibu wa Serikali wa kutoa notisi pale ambapo mtu anakuwa na jambo na Serikali anatakiwa atoe taarifa badala ya kufanya kienyeji bila kufuata utaratibu, "unatakiwa utoe notisi pale ambapo una jambo lako, maoni au kuuliza Serikali vinginevyo utakutana na mabingwa wa sheria watakukumbusha utaratibu," amesisitiza Balozi Chana.

Ameielekeza OWMS kuwa tayari kupokea Ofisi zote za Serikali na kuwapa ushauri stahiki ili taratibu ziweze kuzingatiwa na Serikali isiingie kwenye hasara yeyote itakayosababisha upotevu wa fedha za Serikali. Amesisitiza Ofisi za Serikali zizingatie sheria, taratibu na miongozo hususani kwenye masuala yote ya madai na wapate ushauri ili kulinda maslahi ya Serikali na nchi kwa ujumla.

Ameongeza kuwa milango ya Wizara ya Katiba na Sheria ipo wazi, hivyo taasisi za Serikali zinapokuwa na masuala wasisite kuwasiliana na Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na OWMS kwa kuwa kazi yetu ni kuwashauri, kuwasikiliza, kuwapa maoni na kuwakumbusha kuhusu utaratibu wa mashauri ili pale mtu anapokuwa na haki yake izingatiwe kwani sisi tumeapa kulinda haki za watanzania na taasisi.

Akitoa taarifa kwa niaba ya OWMS, Wakili Mkuu wa



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akipokea jarida, nyaraka na zawadi kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende alipotembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam katika ziara ya kikazi. Anayeshuhudia ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Pauline Gekul (Mb).*

Serikali, Dkt. Boniphace Luhende amesema kuwa OWMS ina jukumu la kuendesha mashauri mbalimbali ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake. Aliongeza kuwa OWMS pia inashiriki kuendesha mashauri yanayohusu kampuni ambayo Serikali ina hisa, kwa mfano hivi karibu imeendesha shauri la benki ya CRDB lenye thamani ya shilingi bilioni 33.

Dkt. Luhende ameongeza kuwa tangu kuanzishwa kwake OWMS imeweza kumaliza mashauri mbalimbali kwa njia ya majadiliano, ikiwemo shauri lililohusu ujenzi wa SGR lililofunguliwa nchini Rwanda. Pia, OWMS imeendesha shauri lililofunguliwa Baraza la Usuluhishi la London ambapo Serikali ilikuwa inadaiwa shilingi trilioni saba na kufanikiwa kumaliza shauri hilo kwa majadiliano. Hivyo, kuwezesha Serikali kuepuka kulipa fedha hizo.

Amesema kuwa pamoja na OWMS kushinda katika kuendesha mashauri kwa majadiliano nje ya mahakama, OWMS imekuwa inakabiliana na changamoto mbalimbali kama vile baadhi ya taasisi za Serikali kuvunja mikataba au makubaliano ya kisheria waliyoingia na mtoa huduma au mkandarasi bila kuishirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hivyo kuzalisha migogoro inayokiuka sheria za mikataba, baadhi ya taasisi za Serikali zinachelewesha malipo ya huduma kwa wakandarasi hivyo kupelekea kufunguliwa kwa mashauri ya madai dhidi ya Serikali ambapo miradi hiyo ingesimamiwa vizuri ingeepuka milolongo ya kuiingiza Serikali katika madai na migogoro isiyoisha na baadhi ya taasisi kushindwa kutoa au kutoa ushirikiano hafifu wakati wa kuandaa nyaraka mbalimbali zinazohitajika mahakamani




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akiangalia vitabu, nyaraka na majarida mbalimbali yaliyopo kwenye Maktaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara yake kwenye Ofisi hiyo Jijini Dar es Salaam.*

na usimamizi hafifu wa miradi hasa miradi ya ujenzi ambayo imepelekea kuleta migogoro inayoenda kwenye suala la usuluhishi.

Hali kadhalika, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana ameitaka OWMS na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuzikumbusha taasisi za Serikali, Ofisi za halmashauri, Wilaya, kata na vijiji vyote na watendaji wote nchi nzima kuzingatia utawala bora, misingi ya sheria na haki ili wananchi wanapokuwa na maswali au wanahitaji ufahamu kwenye masuala mbalimbali kama mirathi, ardhi na ushauri wa masuala ya madai wajibiwe kwa wakati. Mhe. Waziri Balozi Dkt. Pindi Chana amesisitiza kuwa Mhe. Rais Dkt. Samia ameweka Ofisi hizi kwa ajili ya watanzania hivyo ni muhimu kwa watanzania kufahamu haki zao na wasiwe wanyonge.



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende alipowasili Ofisini kwake wakati wa ziara yake kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akizungumza na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipotembelea Ofisi hiyo akiwa kwenye ziara yake ya kikazi Jijini Dar es Salaam.*




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia viongozi mbalimbali na wananchi katika Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nanenane Kitaifa yaliyofanyika kwenye viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya tarehe 8 Agosti, 2023.*

# Rais Dkt. Samia: Ongezeni Tija na Ubunifu katika Shughuli za Kilimo

Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan , ametoa wito kwa wakulima nchini kuongeza tija na ubunifu katika shughuli za kilimo ambapo amesema Serikali itaendelea kuweka mazingira bora na wezeshi ili kuhakikisha kilimo kinawakwamua wakulima kimaisha nchi nzima.

Rais Dkt. Samia amesema hayo tarehe 08 Agosti, 2023 wakati akihitimisha sherehe za Kilele cha Maonesho ya kimataifa ya Kilimo Nanenane yaliyofanyika uwanja wa John Mwakangale Jijini Mbeya.

Akizungumza na wananchi walioshiriki kilele cha maonesho hayo Rais Dkt. Samia amesema kuwa, miongoni mwa juhudi zilizofanywa kuboresha kilimo ni pamoja na kuanzishwa kwa Programu ya Miaka 8 ya Kujenga Kesho Bora ya Vijana ijulikanayo kama ***Building Better Tomorrow (BBT)*** inayolenga kuhamasisha vijana kufanya kilimo cha kisasa kwa lengo ya kujikwamua kiuchumi kwa wao wenyewe na Taifa kwa ujumla.

Aidha, Mhe. Dkt. Samia ametumiamaadhimishohayo kuelezea umati wa wananchi walioshiriki maonesho hayo na watanzania kwa ujumla kuwa Serikali yake haijazuia wananchi hususan wakulima kuuza mazao nje ya nchi bali inawataka wazingatie utaratibu mzuri wa kusafirisha mazao ikiwa ni pamoja na wakulima kuuza mazao yao kupitia kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula hatua itakayosaidia kuondoa uuzaji wa mazao hayo nje ya nchi kiholela.

Katika hatua nyingine Rais Dkt. Samia, ameielekeza Wizara ya Kilimo kuangalia uwezekano wa kuvuta maji kutoka kwenye maziwa na kuyapeleka kwa wakulima kwaajili ya kusaidia kilimo cha umwagiliaji ambapo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza uzalishaji wa chakula cha kutosha hasa katika maeneo yasiyopata mvua za kutosha kwa mwaka.

Kupitia maadhimisho hayo Rais Dkt. Samia ameshuhudia utiaji saini wa mkataba wa Programu ya Kujenga Kesho Bora ya Vijana (BBT) baina ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya mifugo na Uvuvi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambapo vijana hao watapata fursa ya kujengewa uwezo katika masuala ya kilimo pamoja na kupewa elimu ya uzalendo kwa mwezi mmoja.

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amehitimisha kilele cha Maonesho ya Kimataifa ya Nanenane kwa kuzindua programu ya uchimbaji visima 67,800 kwa wakulima wadogo nchi nzima, ugawaji wa vishikwambi kwa maafisa ugani, utoaji wa vifaa vya kutengeneza vihenge kwa wakulima nchi nzima, makala ya miradi ya umwagiliaji, usanifu wa uwanja wa kisasa wa maonesho ya kilimo.

Kwa upande wake Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo amesema kuwa Ofisi itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali katika utatuzi wa migogoro ikiwemo migogoro yote inayohusiana na masuala ya ardhi.

Akizungumzia dhumuni la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kushiriki Maonesho hayo, Mwaipopo amesema kuwa, Ofisi imeshiriki maadhimisho hayo kwa kuwa inasimamia utatuzi wa migogoro na moja kati ya migogoro ambayo imejitokeza kwa kiasi kikubwa ni pamoja na migogoro ya ardhi ambayo inahusiana na maonesho ya Nanenane.

Ameongeza kuwa ili kuwa na chakula cha kutosha na chenye usalama Ofisi itaendelea kutatua migogoro hiyo hatua itakayosaidia kuongeza uzalishaji wa chakula cha kutosha kwa kuwa uwepo wa migogoro ya ardhi nchini umechangia kupunguza uzalishaji hasa wa chakula katika maeneo mbalimbali nchini.




*Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan , akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa ugawaji wa vitendea kazi kwa Maafisa Ugani, bei elekezi ya mbolea, uchimbaji wa visima ,vifaa vya umwagiliaji pamoja na vifaa vya ujenzi wa vihenge kwa vijana.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika kwenye viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya.*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akisaini Kitabu cha wageni alipowasili kwenye banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Mbeya.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili kwenye banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Mbeya.*




*Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na watumishi wa Wizara hiyo na wananchi waliotembelea banda la Wizara hiyo wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Mbeya.*




*Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Jaji Mstaafu Mhe. Mathew Mwaimu (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) alipotembelea banda la Ofisi hiyo kwenye Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Mbeya. Wa pili kulia ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo.*




*Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Wizara ya Katiba na Sheria alipotembelea Banda la Ofisi hiyo katika Maonesho ya Nanenane yanayoendelea Jijini Mbeya.*




*Naibu Kabidhi Wasii Mkuu, Bi. Irene Lesulie akisaini kitabu cha wageni alipotembelea Banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Maonesho ya Nanenane yanayoendelea Jijini Mbeya.*




*Mkurugenzi Msaidizi Udhibiti Ubora, Bi. Mercy Kyamba akielezea majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mwananchi alipotembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Mbeya.*




# *Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria Kuleta Usawa Nchini*

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo ameiwakilisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kwenye uzinduzi wa Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria iliyozinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango mjini Songea yenye kauli mbiu isemayo, "***Msaada wa Kisheria kwa Haki, Usawa, Amani na Maendeleo,***" ambapo imehudhuriwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb).

Bi. Mwaipopo amesema kuwa sisi kama OWMS tayari tupo kwenye mikoa kumi na saba ikiwemo mkoa huu wa Ruvuma ambapo leo tumeshuhudia tukio hili likizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango na tunatarajia kushiriki kikamilifu katika siku tisa zijazo ambazo Kampeni hii itatekelezwa mkoani Ruvuma.

> ***"Msaada wa Kisheria kwa Haki, Usawa, Amani na Maendeleo"***

Sisi tuna amini katika kauli mbiu ya Kampeni hii ambayo inasema, "*Msaada wa Kisheria kwa Haki, Usawa, Amani na Maendeleo,*" tunasema kwamba Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria ni chachu na nguzo katika kuleta maendeleo nchini ili kuleta usawa na amani Tanzania

Bi. Mwaipopo amesema kuwa ushiriki wetu unahusisha uwepo wa banda la maonesho katika uwanja wa Majimaji ambapo Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ruvuma, Egidy Mkolwa watakuwa wakiwahudumia wananchi wa Ruvuma wenye matatizo ya kisheria, kuwasikiliza na kuwashauri cha kufanya na mahali pa kwenda ili waweze kutatua matatizo yao.

OWMS ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na tumeshiriki kikamilifu Kampeni hii ambayo inalenga kuhakikisha kuwa taasisi za Serikali kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia na nyinginezo tunatekeleza Kampeni hii ya miaka mitatu kwa kuhakikisha kwamba wananchi wanyonge wa Tanzania, watoto, wanawake, wale ambao hawana uwezo wa kupata msaada wakisheria kwa gharama nafuu wanahudumiwa kupitia Kampeni hii.

Ofisi ya Wakili wa Serikali ina Ofisi zake kwenye mikoa kumi na saba nchini ikiwemo Dar es Salaam, Dodoma, Ruvuma, Tanga, Arusha, Mwanza, Rukwa, Kagera, Mara, Tabora, Iringa, Morogoro, Mtwara, Kilimanjaro, Shinyanga, Mbeya na Kigoma ambayo inahusika kwenye mnyororo wa utoaji haki nchini hivyo ushiriki wake kwenye maonesho inaipa fursa OWMS kupata changamoto za wananchi, kuwaelimisha na kufanyia kazi malalamiko yanayohusu taasisi za Serikali.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akimkabidhi Jarida la Wakili Mkuu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mhe. Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu alipotembelea banda la maonesho la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria mjini Songea.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mercy Kyamba akitoa maelezo kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango alipotembelea banda la Ofisi hiyo kabla hajazindua Kampeni ya Msaada wa Kisheria mjini Songea. Wa kwanza kulia ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb).*



*Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Songea, Mhe. Japhet Manyama akipata maelezo kutoka Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, James Kibamba kuhusu majukumu ya Ofisi hiyo alipotembelea banda la maonesho la Ofisi hiyo wakati wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria iliyofanyika mjini Songea.*




*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ruvuma, Egidy Mkolwe (wa kwanza kulia) wakihudumia wananchi kwenye banda la Ofisi hiyo wakiwapatia elimu kuhusu masuala ya kisheria wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria iliyozinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango mjini Songea.*




*Mwananchi akifurahia jambo kwenye banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kupatiwa elimu ya kisheria na Mawakili wa Serikali wa Ofisi hiyo wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria iliyozinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango mjini Songea.*



*Wanachi wakimsikikiza kwa makini Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akihutubia wananchi hao kabla hajazindua Kampeni ya Msaada wa Kisheria mjini Songea. Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Sarah Mwaipopo (hayupo pichani).*




*Waziri Mkuu Kassim Majaliwa afungua Maonyesho ya Sabasaba*




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akizungumza na wananchi (hawapo pichani) wakati akifungua Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa, yanayofanyika kwenye Viwanja vya Maonesho vya Sabasaba Kurasini jijini Dar es Salaam.*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) ametoa wito kwa wafanyabiashara kote nchini kutumia maonesho ya 47 ya biashara ya kimataifa ya Sabasaba pamoja na fursa zilizopo ili kujifunza kuhudumia masoko makubwa ya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Majaliwa ametoa wito huo Julai 05, 2023 wakati akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ufunguzi wa maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa kwa mwaka 2023 yaliyofanyika katika Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.

Ameongeza kuwa kufunguka kwa Soko la Eneo Huru la Afrika ambalo linakadiriwa kuwa na walaji zaidi ya bilioni 1.3 kutoka nchi 53 za Afrika ni fursa kubwa kwa wafanyabiashara wote wa Tanzania hivyo niwaombe wale wote wenye bidhaa zenye viwango na wanaoweza kukidhi vigezo kujisajili kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ili kunufaika na mpango huo.

"***Niwaombe wale wote wenye bidhaa zenye viwango na wanaoweza kukidhi vigezo kujisajili kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ili kunufaika na mpango huo. Ni muhimu sana tukaweka jitihada za dhati kuyafikia masoko haya na siyo kuwa waangaliaji tu na kulalamika,***" alisisitiza Mhe. Majaliwa.

Aidha, amezitaka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara zishirikiane na Wizara ya Kilimo katika kuandaa mpango wa pamoja kuhakikisha uzalishaji unafanyika kwa kuzingatia mahitaji ya masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kuwa Wizara hizi mbili lazima zisomane kiutendaji sambamba na



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akiangalia asali inayozalishwa na Kampuni ya Pinda Honey katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Waziri Mkuu Mstaafu, Mhe. Mizengo Pinda.*

kuwashirikisha kikamilifu wataalam wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania katika kutekeleza majukumu ya ufunguaji wa fursa za masoko ndani na nje ya nchi.

Katika hatua nyingine Mhe. Majaliwa ameipongeza Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania kwa kutenga eneo maalum kwa ajili ya wamachinga ili nao waweze kufanya biashara kwa uhuru na utulivu zaidi sambamba na kujifunza mbinu za kukua kibiashara hatimaye waweze kukuza mitaji yao na kutumia fursa zitakazopatikana kwa ufasaha zaidi.

Ameeleza kuwa ni muhimu kwa wafanyabishara wadogo wadogo maarufu kama wamachinga nchini kujifunza matumizi ya teknolojia na mbinu za ufanyaji wa biashara hatua itakayowasaidia kukua zaidi.

Katika kuhakikisha lengo la kukuza biashara zao linatimia Mhe. Majaliwa amezitaka halmashauri nchini kote kuweka utaratibu mzuri wa kuwapanga wamachinga katika maeneo rafiki kibiashara, ili wafanye biashara zao kwa uhuru hatua itakayosaidia kuchangia uchumi kikamilifu kupitia ulipaji wa kodi kwa lengo la kukuza pato la taifa kwa ujumla.

Amesema ni vyema sasa maeneo ya wamachinga yakawekewa miundombinu yote muhimu ikiwemo miundombinu ya maji na umeme kwa kuwa hatua hii itasaidia kuwainua wafanyabiashara hao kutoka kuwa wafanyabiashara wadogo wadogo, wakati na hatimaye kuwa wafanyabiashara wakubwa.

Akizungumza katika ufunguzi wa maonesho hayo, Naibu Waziri wa Uwekezaji na Viwanda, Mhe. Exaud Kigahe (Mb) amesema Maonesho hayo ni nyenzo muhimu katika kuwakutanisha wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya nchi na kuwapa nafasi ya kutengeneza mitandao ya kibiashara pamoja na kupata masoko zaidi ya bidhaa na huduma wanazozalisha hatua ambayo imewasaidia kupata masoko ya uhakika pamoja na kukuza mitaji yao.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Olingeta Mbamba amesema Mamlaka hiyo pamoja na mambo mengine imefanikiwa kushirikiana na Ofisi za Balozi katika nchi za Kenya na Malawi kuratibu wafanyabiashara 206 kutoka Tanzania katika misafara ya kibiashara katika nchi za Sudani Kusini na Malawi ambayo imeweza kutangaza fursa kwa wafanyabiashara wa Tanzania.

Maonesho hayo ya 47 ya Biashara ya Kimataifa yanahusisha Wizara, Taasisi, Idara, Mikoa, Halmashauri na sekta binafsi yakiwa na kauli mbiu isemayo, "***Tanzania Mahali Sahihi Pa Biashara na Uwekezaji,***" ambapo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inashiriki Maonesho haya kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akitembelea mabanda katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Manonesho vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam.*



*Wakili wa Serikali, Evelius Mwendwa akitoa maelezo kuhusu majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mwananchi alipotembelea Banda la Ofisi hiyo kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.*




*Afisa Habari wa Mahakama ya Tanzania, Bi. Mary Gwera akisaini kitabu cha wageni alipotembelea Banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa 2023 yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam akihudumiwa na Wakili wa Serikali wa Ofisi hiyo, Bi. Rehema Mtulya.*




*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Hosana Mgeni akipitia nyaraka ya mwananchi aliyetembelea banda la Ofisi hiyo kwa lengo la kupata msaada wa kisheria katika maonesho ya Biashara ya Kimataifa yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.*




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Kassim Majaliwa akitembelea mabanda katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara, yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Manonesho vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam.*




**Prof. Ibrahim Hamis Juma**
Jaji Mkuu wa Tanzania

# *Jaji Mkuu Ataka Mawakili Kubadilika Kifikra*

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma amewahimiza Mawakili wapya waliopokelewa kubadilika kifikra, mitazamo na mbinu za utoaji wa huduma ili kuziona fursa za ajira ambazo zinaibuliwa katika karne ya sasa.

Prof. Juma ameyasema hayo katika sherehe ya 68 ya kuwakubali na kuwapokea Mawakili wapya 195 iliyofanyika tarehe 6 Julai, 2023 kwenye Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam, ambapo idadi hiyo imefanya mpaka sasa kuwa na Mawakili wanaofikia 11,637 nchi nzima.

"*Mkiganda katika zama ziliyozopita, zama zinazotokana na aina ya masomo tunayopata Chuo Kikuu na Shule ya Sheria tutakosa hizo fursa na hivyo kubaki watu tunaolalamika mara kwa mara,*" amesema Jaji Mkuu.

Jaji Mkuu amesema kuwa umefika wakati sasa Mawakili na Wanasheria vijana kukubali ukweli kuwa

Elimu ya Sheria waliyopata Vyuo Vikuu na Shule ya Sheria, haikuwatayarisha kukabiliana na changamoto ya kutafuta fursa zinazoibuliwa na mabadiliko katika Karne ya 21 hivyo amewasihi Mawakili hao kutumia fursa zilizopo sasa kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa na Serikali ama kampuni binafsi.

Amesema kuwa ni vizuri kwa Mawakili waliokubaliwa na kupokelewa leo kujiweka katika hali ya kusoma fursa katika mabadiliko mbalimbali ambayo yanatokea katika jamii tuliyonayo leo kwa kuwa wasipoelewa dunia ambayo inawazunguka fursa hizo hawataziona wala kuwafuata nyumbani kama ilivyokuwa zamani ambapo wahitimu wa kada mbalimbali waliajiriwa moja kwa moja.

Mhe. Prof. Juma amesisitiza kuwa Mawakili wanatakiwa kuwa na miwani ambayo ni tofauti na miwani waliyoizoea, miwani ambayo itaweza kuona fursa ambazo watu wengine hawazioni.

"*Mawakili wapya hamuwezi kuziona fursa mpya za karne ya 21 kama mitazamo yenu, tamaduni na uelewa wenu wa sheria ni kupitia miwani na maudhui ya dunia ya karne za 19 na 20,*" amesema Jaji Mkuu.

Ameongeza kuwa huwa anafuatilia mijadala katika mitandao ya kijamii, kwa bahati mbaya amegundua bado Wanasheria na Mawakili wa Tanzania wanajenga hoja zao kwa kutumia uoni na miwani ya zamani isiyoweza kuona fursa zilizozalishwa na utandawazi na ukuaji mkubwa wa matumizi ya teknolojia.

Jaji Mkuu amebainisha pia kuwa Wanasheria na Mawakili bado hawajaweza kuona fursa kubwa tarajiwa kutoka kwenye miradi mikubwa ya uwekezaji, mfano Reli ya Kisasa ya Mwendokasi (SGR) na Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere ambazo zinalenga kufungua fursa za ajira sio tu ndani ya Tanzania bali pia nchi nyiingine katika Bara la Afrika.

"*Juzi nikiwa Namibia, nilipata nafasi ya kuongea na Mawakili wa huko, wao ujenzi wa SGR wanaona ni fursa na tayari wameanza*




*Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma akiwa kwenye picha ya pamoja na la Mawakili wakiongozwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (wa tatu kulia) mara baada ya sherehe ya kuwakubali na kuwapokea Mawakili wapya 195 iliyofanyika kwenye Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam. Watatu kutoka kushoto ni Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende.*

*kuangalia ni namna gani watakuja kutoa huduma hapa Tanzania. Wanaposikia kuwa kuna bwawa kubwa la umeme ambalo litaibua viwanda, wao kama Mawakili wanasema kwao ni fursa ambayo itawaunganisha Tanzania na nchi nyingine za kiafrika na hata duniani kote,"* amesema Jaji Mkuu.

Jaji Mkuu Mhe. Prof. Ibrahimu Hamis Juma amewaomba Mawakili hao kubadilisha mitazamo na fikra zao wao wenyewe huku wakijiendeleza kwa kuvaa miwani yenye uwezo wa kuona hizo fursa.

Akitolea mfano katika kitabu cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin William Mkapa kiitwacho "***My Life My Purpose***" katika ukurasa 96, Prof. Juma amemnukuu akisema, "***We Must Change Ourselves or We Will Be Changed,***" akimaanisha kuwa, "*Ni Lazima Wanasheria na Mawakili tujibadilishe kifikra, kimtazamo na kinyakati, vinginevyo tutalazimishwa kubadilika.*"

Kuhusu nafasi ya vijana katika kutoa huduma Prof. Juma amesema kuwa vijana ndio kundi lenye muda mrefu zaidi wa kutoa huduma, hivyo amelitaka kundi hilo kutokutegemea sana Mawakili ambao tayari wanazo ajira kwa kuwa sio rahisi kuwazungumzia matatizo yao.

"*Ninyi ndiyo mnatakiwa kuibua hizo fursa, kwa sababu wale ambao wanazo hawatakuwa na nia ya kuongelea changamoto ya ajira ambayo inawakumba Mawakili wanaoingia katika soko la ajira,*" amesema Jaji Mkuu.

Jaji Mkuu amebainisha pia kuwa katika miaka ya hivi karibuni, masuala yanayozungumziwa katika Mikutano ya Jukwaa ya Majaji Wakuu wa Nchi za Afrika Kusini na Mashariki ya Afrika ni kielelezo tosha kuwa Mahakama Barani Afrika zimeamua kubadilisha fikra na mitazamo hatua ambayo imesaidia kukabiliana na changamoto zinazokabili nchi zetu katika Karne ya 21 ambazo ni tofauti na changamoto zilizokuwepo kuanzia miaka ya uhuru mwaka 1960 hadi ya Karne ya 21.

Sherehe za kuwakubali na kuwapokea Mawakili wapya imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Majaji wa Mahakama ya Rufani na wale wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Dkt. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi, Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende na viongozi wengine wa Serikali.




*Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma(aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mawakili wapya 195 mara baada ya kukubaliwa na kupokelewa katika sherehe iliyofanyika katika Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam.*



*Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Shamillah Sarwatt akiongoza kiapo cha uadilifu kwa Mawakili wapya 195 waliopokelewa na Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma katika sherehe iliyofanyika katika Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam.*



*Sehemu ya Mawakili wapya waliokubaliwa na kupokelewa wakila kiapo cha uaminifu mbele ya Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma katika sherehe iliyofanyika katika Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam.*



*Sehemu ya Mawakili wapya waliokubaliwa na kupokelewa wakimsikiliza Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma (hayupo pichani) mara baada ya sherehe ya kuwakubali na kuwapokea Mawakili hao iliyofanyika katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam.*



*Baadhi ya Mawakili wapya wakifurahia jambo mbele ya Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma (hayupo pichani) mara baada ya kuwakubali na kuwapokea Mawakili hao kwenye hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza na Mawakili wa Serikali wa Mkoa wa Iringa (hawapo pichani) akiwa ziarani mkoani humo kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mkoa wa Iringa. Kulia ni Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Mkoa wa Iringa, Ansila Makyao.*

# Mawakili wa Serikali Washirikishwe Kikamilifu katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Kuzuia Migogoro

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo amefanya ziara ya kikazi kwenye Ofisi za Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) zilizopo Mikoa ya Ruvuma na Iringa kwa lengo la kukagua utendaji kazi wa Ofisi hizo. Katika ziara hiyo, alifanya vikao na Mawakili wa Serikali wa Manispaa, Halmashauri na Ofisi za Mkuu wa Mkoa, wanaotekeleza majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Aidha, Bi. Mwaipopo alitembelea Mahakama Kuu Kanda ya Songea na Iringa na kupata fursa ya kufanya majadiliano na Majaji Wafawidhi kuhusu mashauri yanayoendeshwa katika Kanda hizo za Makahama yanayosimamiwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Katika ziara hiyo, Bi. Mwaipopo akiongea kwa niaba ya Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali, amewapongeza Mawakili wa Serikali kwa ushirikiano na kazi nzuri wanayoifanya ya usimamizi wa mashauri yanayofunguliwa na/au dhidi ya Serikali. Aidha,

amesisitizia umuhimu wa Mawakili wa Serikali kusimamia mashauri kwa ufanisi na kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu, miongozo na Hati Idhini ya uendeshaji mashauri zinazotolewa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Amewataka Mawakili wa Serikali kutoa taarifa kwa wakati za mashauri yote yanayofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali, kutoa ushirikiano kwenye Ofisi wakati wa uandaaji wa mashauri, ushahidi na mashahidi wao wakati wa uendeshaji mashauri mahakamani.

Bi. Mwaipopo amewakumbusha Mawakili kuhakikisha wanakuwa vinara wa kuzuia migogoro inayoweza kujitokeza katika utendaji na utekelezaji wa miradi mbalimbali na kuzalisha kesi dhidi ya Serikali kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anapeleka fedha nyingi kwenye mikoa na halmashauri mbalimbali nchini ili kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Pia, ameongeza kuwa ushiriki na ushirikishwaji wa Mawakili wa Serikali ni muhimu kwenye hatua zote za uaandaji na utekelezaji wa mikataba kwa lengo la kuzuia migogoro inayoweza kuigharimu Serikali kuendesha mashauri na kulipa fidia kwa kadri vyombo vya haki vitakavyoelekeza. Amewakumbusha Mawakili kuzingatia sheria, kanuni na taratibu wakati wa uandaaji na upekuzi wa mikataba na kuhakikisha wanashirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kikamilifu



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Songea Mhe. Jaji Ephery Sedekia (katikati) na Wakili wa Serikali Mfawidhi, Egidy Mkolwe akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi hiyo mkoani humo.*

na kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi wakati wa kikao cha Mawakili wa Serikali kilichofanyika Septemba mwaka 2022 kwa lengo la kuzuia migogoro inayoweza kujitokeza kwa taasisi kutokufuata taratibu katika utekelezaji wa majukumu.

Katika hatua nyingine, Bi Mwaipopo aliwasisitizia Mawakili wa Serikali kufanya vikao vya mara kwa mara vya pamoja na OWMS za Mikoa kwa lengo la kutathmini utendaji kazi wa mashauri yanayofunguliwa mikoani, mafanikio na changamoto wanazozipitia katika utekelezaji wa majukumu ya uendeshaji mashauri.

Pia, alipata fursa ya kufanya mazungumzo na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Songea, Mhe. Ephery Sedekia na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Iringa, Mhe. Ilvin Mugeta kwa kuwa OWMS inashirikiana na kufanya kazi kwa karibu na Mahakama hizo kwenye kazi za uendeshaji wa mashauri. Mazungumzo hayo pia yalihusisha mifumo ya usimamizi wa mashauri baina ya taasisi hizo ambayo inapaswa kusomana ili kuhakikisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati pamoja na ufanyaji wa tafiti wa mashauri ambayo yanafunguliwa kwa wingi kwa mfano mashauri ya ardhi, kwa lengo la kuishauri Serikali na taasisi zake.

Waheshimiwa Majaji Mugeta na Sedekia wamesema kuwa OWMS inawapa ushirikiano wa kutosha katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali na taasisi zake, jambo ambalo limeiwezesha Serikali kupata mafanikio katika mashauri ambayo yanaendeshwa na kukamilika.

Halikadhalika katika ziara hiyo, Bi. Mwaipopo ameonana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Steven mashauri na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Bashir Muhoja na kuahidi kuendeleza ushirikiano kwenye maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu.

Mawakili wa Serikali Wafawidhi, Mikoa ya Ruvuma na Iringa, Egidy Mkolwe na Ansila Makyao, wameishukuru OWMS kwa kuwapatia ushirikiano, magari na vitendea kazi ambavyo vinawawezesha kutekeleza majukumu ya kuendesha mashauri ya Serikali ndani ya Mikoa wanayofanyia kazi

Bi. Mwaipopo amewaahidi Mawakili wote wa Serikali kuwa OWMS kwa kushirikiana na mamlaka nyingine ndani ya Serikali itaendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha kwenye masuala ya uendeshaji mashauri na mengineyo yanayohusiana na kufanya ziara endelevu za utendaji kazi ili kuhakikisha kuwa sheria, taratibu na kanuni zinazingatiwa katika mnyororo wa utoaji haki.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akifurahia jambo na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Iringa, Mhe. Ilvin Mugeta Ofisini kwake akiwa ziarani kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa humo. Kushoto ni Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Mkoa huo, Ansila Makyao.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza na Mawakili wa Serikali kutoka Sekretarieti za Mikoa, Jiji, Miji, Wilaya na taasisi za Serikali kutoka Mkoa wa Mbeya na Songwe Katika kikao chenye lengo la kufahamu namna Mawakili hao wanavyotekeleza majukumu yao ya kila siku.*

# Mwaipopo: Tekelezeni Majukumu Yenu kwa Kufuata Miongozo Iliyowekwa na Serikali

Mawakili wa Serikali kutoka Sekretarieti za Mikoa, Jiji, Miji, Halmashauri na Taasisi za Serikali katika mkoa wa Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi wametakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia miongozo iliyowekwa na Serikali hatua itakayosaidia kutimiza malengo waliyojiwekea kwa wakati.

Wito huo umetolewa na Naibu wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo wakati akizungumza na Mawakili hao katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na ule wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi mkoani Rukwa kwa lengo la kujadili na kufahamu namna wanavyotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Amesema kuwa kufanya kazi kwa kufuata miongozo ya Serikali hasa mwongozo wa kuendesha, kuratibu na kusimamia mashauri ya Serikali uliotolewa mwaka 2021 na Wakili Mkuu wa Serikali utawasaidia Mawakili wa Serikali kuendesha mashauri ya Serikali kwa weledi na ufanisi zaidi hatua itakayosaidia Serikali kushinda mashauri mengi na kuokoa fedha ambazo zitaelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa manufaa ya

Taifa.

Aidha, kiongozi huyo amewasihi Mawakili hao kuwa na jukwaa la pamoja litakalokuwa na jukumu la kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria pamoja na kujadili mbinu mbalimbali za uendeshaji wa mashauri ya Serikali ikiwa ni pamoja na kujadili na kutatua changamoto zinazowakabili katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali kwa kushirikiana na Ofisi.

Akizungumza kuhusu mafunzo kwa Mawakili, Bi. Mwaipopo amesema kuwa Ofisi yake itaendelea kuendesha mafunzo kwa Mawakili wa Serikali ikiwa ni pamoja na kushirikisha Mawakili wengi zaidi kulingana na bajeti itakavyoruhusu ili kuwawezesha Mawakili wote nchini waweze kupata mafunzo hayo ambayo yamewasaidia kwa kiasi kikubwa kuwaongezea mbinu mbalimbali katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali.

Kupitia kikao hicho, Bi. Mwaipopo amewataka kuendelea kushiriki mafunzo hayo kwa kuwa mafunzo hayo ndio jukwaa litakalosaidia kuwajengea uwezo katika uendeshaji wa mashauri kwa ufanisi na weledi zaidi.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Madai Mark Mulwambo, amewashukuru Mawakili hao kwa kazi nzuri wanayofanya huku akiwasihi kuendelea kushauri namna



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (aliyesimama katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali wa Sekretarieti za Mikoa, Jiji, Miji, Wilaya na Taasisi za Serikali kutoka Mkoa wa Mbeya na Songwe mara baada ya kumalizika kwa kikao kilichokuwa na lengo la kujadili namna Mawakili hao wanavyotekeleza majukumu yao.*




*Mkurugenzi wa Idara ya Madai Mark Mulwambo akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wa Sekretarieti za Mikoa, Jiji, Miji, Wilaya na Taasisi za Serikali kutoka Mkoa wa Mbeya na Songwe wakati wa kikao kilicholenga kufahamu namna Mawakili hao wanavyotekeleza majukumu.*

bora ya kuendesha na kusimamia mashauri ili Serikali iendelee kushinda mashauri yake katika Mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Amewakumbusha Mawakili hao kuendelea kutuma taarifa za mashauri wanayoyasimamia kila mwezi ili Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iweze kutathimini na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuongeza nguvu katika yale mashauri yenye maslahi mapana kwa lengo la kuisaidia Serikali kuendesha mashauri hayo kwa ufanisi zaidi.

Naye Mkurugenzi Msaidizi Udhibiti Ubora, Bi. Mercy Kyamba, amewakumbusha Mawakili kujisajili kwenye mfumo wa kuratibu taarifa za Mawakili wa Serikali unaosimamiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa kufanya hivyo itawasaidia kutambuliwa na kutekeleza majukumu yao pasipo changamoto zozote.

Akizungumza kwa niaba ya Mawakili hao, Wakili wa Serikali Mkuu kutoka TARURA Kanda ya Mbeya Bakari Bakari amemshukuru Bi. Mwaipopo kwa kuandaa kikao hicho huku akiahidi kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi zaidi ikiwa ni pamoja na kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa kwa lengo la kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi zaidi.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo ametumia ziara hiyo kuwatembelea viongozi mbalimbali wa Serikali akiwemo Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga Mhe. Amir Mruma, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Sumbawanga Mhe. Thadeo Mwenempanzi, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa Mhe. Makongoro Nyerere na Katibu Tawala Mkoa wa Rukwa, Gerald Kussaya.



*Joseph Tibaijuka wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mbeya akitoa neno la shukrani mara baada ya kikao baina ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo na Mawakili wa Serikali kutoka Sekretarieti za Mikoa, Jiji, Miji, Wilaya na taasisi za Serikali kutoka Mkoa wa Mbeya na Songwe wakati wa kikao kilicholenga kufahamu namna Mawakili hao wanavyotekeleza majukumu yao.*



*Mawakili wa Serikali kutoka Sekretarieti za Mikoa, Jiji, Miji, Wilaya na Taasisi za Serikali kutoka Mkoa wa Mbeya na Songwe wakimsikiliza Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo (hayupo pichani) wakati wa kikao kilicholenga kufahamu namna Mawakili hao wanavyotekeleza majukumu yao.*



*Wakili Wa Serikali wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Peter Salama akielezea namna ambavyo amekuwa akitekeleza majukumu yake wakati wa kikao kati ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (hayupo pichani) kilicholenga kufahamu namna Mawakili hao wanavyotekelza majukumu yao.*

# MATUKIO KATIKA PICHA

## Ruvuma




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akiwa kwenye picha ya pamoja na Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Mkoa wa Ruvuma, Egidy Mkolwe (kulia) na Mkuu wa Mashtaka wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wa Mkoani humo, Kauli Makasi akiwa ziarani mkoani humo kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani humo*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (aliyeketi mbele) akiwa kwenye kikao na Mawakili wa Serikali wa Mkoa wa Ruvuma na baadhi ya Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipokuwa ziarani kukagua utendaji kazi wa Ofisi hiyo mkoani humo*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo akimsikiliza Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Steven mashauri alipofika Ofisini kwake kujitambulisha akiwa ziarani kukagua utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani humo*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akisisitiza jambo akiwa Ofisini kwa Mhe. Jaji Ephery Sedekia, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Songea akiwa ziarani Mkoa wa Ruvuma kukagua utendaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani humo*

# Iringa



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akimsikiliza Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Iringa, Mhe. Ilvin Mugeta (kulia) akizungumza wakati wa ziara yake mkoani Iringa akikagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani humo.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (wa pili kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Iringa, Mhe. Ilvin Mugeta (katikati) akiwa kwenye ziara ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani humo.*

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YASHIRIKI KWENYE KAMPENI YA MAMA SAMIA YA MSAADA WA KISHERIA MKOANI RUVUMA

## UTANGULIZI

Kampeni ya Msaada wa Kisheria inayoitwa "*Mama Samia Legal Aid Campaign*" inatekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria ilizinduliwa Mkoani Dodoma Aprili 27, 2023 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb). Kampeni hiyo imepangwa kufanyika kwa miaka mitatu kuanzia mwezi Machi, 2023 hadi mwezi Februari, 2026 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kampeni hiyo imejikita katika kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi hususan katika masuala ya ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi, mirathi, usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala na masuala yanayohusu haki za binadamu kwa ujumla. Utekelezaji wa kampeni unafanyika kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia, Wanazuoni na Wadau wa Maendeleo.

Lengo kuu la Kampeni ni kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini na katika kufikia lengo hilo, kampeni inaongeza uelewa wa kisheria na haki za binadamu kwa jamii hasa haki za wanawake na watoto; inatoa huduma ya ushauri wa kisheria kwa waathirika na manusura wa ukatili wa kijinsia; kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu elimu ya sheria; masuala ya haki na wajibu na misingi ya utawala



**MERCY KYAMBA**
MKURUGENZI MSAIDIZI UDHIBITI UBORA,
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

bora.

Matokeo ya muda mrefu yanayotegemewa katika Kampeni hii ni kuchangia katika kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wasiojiweza, hususan wanawake, watoto na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Vilevile, itachangia kuimarisha amani na utulivu, kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na kuleta utengamano wa kisiasa hapa nchini.

Matokeo ya kati ni kuimarika kwa mfumo wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria katika ngazi za Serikali Kuu hadi Serikali za Mitaa.

Matokeo ya muda mfupi ni kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotoa taarifa za matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; kupungua kwa idadi ya migogoro na matukio yanayotokana na ukosefu wa uelewa wa sheria; Kuimarika kwa uwajibikaji na uwezo wa taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zinazotoa huduma za msaada wa kisheria.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) ilipata nafasi ya kushiriki katika Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa kisheria katika Mkoa wa Ruvuma wilayani Songea, maadhimisho hayo yalifanyika katika viwanja vya Majimaji yakiwa na Kauli Mbiu isemayo, "***Msaada wa Kisheria kwa Haki, Usawa, Amani na Maendeleo***".

## Masuala Yaliyofanyika Katika Maadhimisho ya Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria

Wizara ya Katiba na Sheria kama mratibu wa kampeni hiyo, waliratibu siku ya ufunguzi wa maadhimisho ambayo ilikuwa ni tarehe 22 Julai, 2023. Katika siku hiyo Mgeni Rasmi alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango.

Wakati wa ufunguzi wa maadhimisho hayo, Mhe. Mpango aliwasisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi kupata ushauri wa kisheria na kutembelea mabanda ili kuweza kupata msaada wa kisheria pamoja na kujua utendaji kazi wa Taasisi husika. Aidha, alizishukuru Taasisi zilizo shiriki na kuwaasa kuwasikiliza wananchi kwa upole ili waweze kutatua matatizo yao.

## Ushiriki wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) ilishiriki kikamilifu katika maadhimisho ya Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria katika viwanja vya Majimaji, Songea. OWMS ilishiriki hususani katika kutoa elimu na ushauri wa kisheria katika eneo la viwanja vya Majimaji ambapo wananchi mbalimbali waliweza kufika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kupata huduma kwa kadiri ya uhitaji wao. Katika banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mawakili wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walitoa huduma ya kisheria kwa kuelimisha wananchi pamoja na kugawa vipeperushi vinavyoelezea Ofisi za Wakili Mkuu wa Serikali sehemu mbalimbali nchini, muundo wa Ofisi, majukumu ya Ofisi pamoja na mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa Ofisi hii mwaka 2018.

Katika Kampeni hiyo, wananchi 41 walihudumiwa ikiwa ni pamoja na wanaume 30 na wanawake 11 walifika kwenye banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata huduma za kisheria.

## Faida za Kushiriki Katika Kampeni

- OWMS imetoa mchango wake kutimiza lengo kuu la Kampeni hiyo ambayo ni kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini;

- Katika kushiriki kwenye kampeni hiyo OWMS imesaidia kuongeza uelewa wa kisheria na haki za binadamu kwa jamii hususan haki za wanawake na watoto;

- Kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu elimu ya sheria, masuala ya haki na wajibu na misingi ya utawala bora.

- kuchangia katika kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wasiojiweza, hasa wanawake, watoto na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi.

- Kuimarisha amani na utulivu kwa wananchi ambapo itasababisha kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na kuleta utengamano wa kisiasa hapa nchini

- Kupunguza uzalishaji wa kesi kwenye Mahakama kwani wananchi watafahamu taratibu nyingine za kiutawala za namna ya kushughulikia changamoto zao kuliko kukimbilia mahakamani kwa kila changamoto wanayokutana nayo.

- U t a p u n g u z a mrundikano wa kesi kwani mwananchi aliyeelimika kuhusu haki zake na sheria ni rahisi kujieleza mahakamani wakati shauri lake linapokuja mahakamani badala ya kuahirisha bila sababu kwa ajili ya kutokuelewa.



*Mkurugenzi Msaidizi wa Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mercy Kyamba akitoa maelezo kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango alipotembelea banda la Ofisi hiyo kabla hajazindua Kampeni ya Msaada wa Kisheria mjini Songea. Wa kwanza kushoto ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb).*



# UTEUZI

Bi. Sarah Mwaipopo aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania tarehe 4 Septemba 2023. Kabla ya uteuzi huo alikuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Bi. Mwaipopo alisoma Shule ya Sekondari ya Kilakala iliyopo Mkoa wa Morogoro ambapo mwaka 1997 alifaulu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es salaam akisomea sheria na kutunukiwa Shahada ya Sheria mwaka 2000.

Mwaka 2003 hadi 2005, Bi. Mwaipopo alijiunga na Chuo Kikuu cha Lund kilichopo nchini Sweden ambapo alisoma Shahada ya Uzamili ya Sheria katika masuala ya haki za binadamu na sheria za kimataifa ambapo alipata weledi kwenye masuala ya haki za binadamu za kimataifa na sheria za kimataifa.

Baada ya mafunzo hayo, Bi. Mwaipopo alifanya mafunzo ya sheria kwa vitendo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,



**Sarah D. Mwaipopo**
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Shirika la Sheria Tanzania na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es salaam. Baadae alijiunga na utumishi wa umma mwezi Januari, mwaka 2001 kama Wakili wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Kurugenzi ya Mashtaka. Mwaka 2002 alihamishiwa

Kurugenzi ya Masuala ya Katiba na Haki za binadamu. Kutokana na utendaji wake mzuri, bidii ya kazi na kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa umma mwaka 2012 alipandishwa cheo kuwa Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Masuala ya Haki za Binadamu, Idara ya Katiba na Haki za Binadamu Ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikali na mwaka 2013 aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa masuala ya Katiba na Haki za Binadamu kwenye Idara hiyo.

Kupitia Idara hiyo, aliratibu masuala mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya katiba, mashauri ya katiba na haki za binadamu kwenye vyombo vya haki vya kitaifa, kikanda na kimataifa kama vile Mahakama ya Kuu ya Tanzania, Mahakama ya Rufani, Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya haki za binadamu na kuiwakilisha nchi kwenye vikao vya Umoja wa Mataifa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwenye masuala mbali mbali ya haki za binadamu.

Katika nyakati tofauti katika kipindi cha Mwaka 2015 na 2016 alikaimu nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa mujibu wa nafasi hiyo alikuwa Mwenyekiti wa Shule ya Sheria kwa Vitendo (Law School of Tanzania).

Mbali na utumishi wake ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bi. Mwaipopo amewahi kuwa Mjumbe wa Sekretarieti ya Bunge la Katiba mwaka 2014, Dodoma. Pia, alikuwa Katibu wa Shirika kwenye Vitengo vya Sheria vya Mamlaka ya EPZA na Shirika la Viwango Tanzania.

Bi Mwaipopo alikuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali na Afisa Masuuli Fungu la 19 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2022 hadi Septemba, 2023 alipoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania ambapo sasa anahudumia umma kama Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Ardhi.

The page reproduces a press release:

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

*Dar es Salaam*
*03 Septemba, 2023*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi kama ifuatavyo:

**a) Uteuzi wa Katibu Mkuu**

Amemteua Balozi Stephen Patrick Mbundi kuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki atakayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki. Balozi Mbundi atachukua nafasi ya Balozi Prof. Kennedy Godfrey Gastorn ambaye ameteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**b) Uteuzi wa Naibu Katibu Mkuu**

Amemteua Balozi Said Shaib Mussa – Balozi wa Tanzania, Kuwait kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Balozi Mussa anachukua nafasi ya Balozi Fatma Rajab ambaye ameteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania, Oman.

**c) Uteuzi wa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Amemteua Balozi Prof. Kennedy Godfrey Gastorn kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Balozi Prof. Gastorn anachukua nafasi ya Dkt. Evaristo Longopa ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

**d) Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani**

i) Amemteua Mhe. Jaji Lameck Michael Mlacha kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi Jaji Mlacha alikuwa Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Kigoma.

ii) Amemteua Mhe. Jaji Paul Joel Ngwembe kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi Jaji Ngwembe alikuwa Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Morogoro.

iii) Amemteua Jaji Mustafa Kambona Ismail kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi Jaji Ismail alikuwa Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Divisheni ya Rushwa na Uhujumu, Dar es Salaam.

iv) Amemteua Jaji Abdul-Hakim Ameir Issa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi Jaji Issa alikuwa Jaji wa Mahakama Kuu, Zanzibar.

**e) Uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu**

i) Amemteua Dkt. Evaristo Longopa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Dkt. Longopa alikuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

ii) Amemteua Bw. Wilbert Martin Chuma kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Chuma alikuwa Msajili Mkuu wa Mahakama ya Rufani Dar es Salaam.

iii) Amemteua Bi. Sharmillah Said Sarwat kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Sarwat alikuwa Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.

iv) Amemteua Bw. Arnold John Kirekiano kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Kirekiano alikuwa Naibu Msajili Mwandamizi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.

v) Amemteua Bi. Martha Boniface Mpaze kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Mpaze alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Jumuishi katika Masuala ya Mirathi na Familia, Dar es Salaam.

vi) Amemteua Bw. Ferdinand Hilali Kiwonde kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Kiwonde alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu.

vii) Amemteua Bw. Said Rashid Ding'ohi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Ding'ohi alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Iringa.

viii) Amemteua Dkt. Angelo Kataraiya Rumisha kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Dkt. Rumisha alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam.

ix) Amemteua Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam.

x) Amemteua Bw. Ntuli Lutengano Mwakahesya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Mwakahesya alikuwa Naibu Karani wa Baraza la Mawaziri, Ofisi ya Rais Ikulu, Dodoma.

xi) Amemteua Bw. Griffin Venance Mwakapeje kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Mwakapeje alikuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Wizara ya Katiba na Sheria, Dodoma.

xii) Amemteua Dkt. Dafina Daniel Ndumbaro kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Dkt. Ndumbaro alikuwa Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dodoma.

xiii) Amemteua Bw. Emmanuel Ludovick Kawishe kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Kawishe alikuwa Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dodoma.

xiv) Amemteua Bw. Abdallah Halfan Gonzi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Gonzi alikuwa Mjumbe wa Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) na Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

xv) Amemteua Bw. Kamazima Kafanabo Idd kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Idd alikuwa Mhadhiri Msaidizi Chuo cha usimamizi wa Fedha (IFM), Dar es Salaam.

xvi) Amemteua Bw. Frank Muyoba Mirindo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Mirindo alikuwa Mhadhiri Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), Tanga.

xvii) Amemteua Bi Hadija Ally Kinyaka kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Kinyaka alikuwa Wakili wa Kujitegemea Kampuni ya Uwakili ya Lawhill Co. & Advocates, Dar es Salaam.

xviii) Amemteua Bi. Aisha Ally Sinda kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Sinda alikuwa Wakili wa Kujitegemea Kampuni ya Uwakili BOWMANS Tanzania, Dar es Salaam.

xix) Amemteua Bw. Hussein Salum Mtembwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bw. Mtembwa alikuwa Wakili wa Kujitegemea na Mmiliki wa Kampuni ya Uwakili ya HM Noble Attorneys, Mtwara.

xx) Amemteua Bi. Irene Daniel Musokwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Kabla ya uteuzi Bi. Musokwa alikuwa Wakili wa Kujitegemea na Mshiriki katika Kampuni ya Uwakili ya FC Attorneys, Dar es Salaam.

Uteuzi huu ni kuanzia tarehe 03 Septemba, 2023.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

## *JAJI MKUU KUONGEZEWA MUDA NI SAHIHI KIKATIBA*

Tarehe 22 Septemba, 2023; Mahakama Kuu (Masijala Kuu) Dar es salaam ilitoa uamuzi katika shauri la Kikatiba Na. 07/2023 baina ya Humphrey Simon Malenga dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutupilia mbali shauri hilo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mahakama imefikia uamuzi huo wa kutupilia mbali shauri hilo (dismissed) kupitia Mhe. Jaji G. N. Isaya kwa sababu zifuatazo:-

***(i) Jaji Mkuu wa Tanzania ana sifa kama Majaji wengine wa Mahakama ya Rufani na hawezi kutenganishwa na Majaji wa Mahakama hiyo kwa mujibu wa ibara ya 118 (2);***

***(ii) Ibara ya 118 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haiwezi kusimama yenyewe kwa sababu inafanya marejeo katika ibara ya 120(1) ambapo ibara ya 120 (1) inasomwa kwa pamoja na ibara ya 120 (2) & (3); na***

***(iii) Mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kumuongezea muda Jaji Mkuu wa Tanzania yalikuwa sahihi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ibara ya 120 (2), (3) & (4) inatumika pia kwa Jaji Mkuu.***

***Hivyo, kitendo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumuongezea muda Jaji Mkuu wa Tanzania hakikuwa kinyume na katiba (it was constitutional).***

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishiriki kwenye Shauri tajwa hapo juu kwa mujibu wa majukumu yake ya kusimamia na kuendesha mashauri ya madai, usuluhishi, katiba, uchaguzi na haki za binadamu kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

23 Septemba, 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

## *OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YAPATIWA MAFUNZO YA UDHIBITI UBORA*

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) wamepatiwa mafunzo ya udhibiti ubora na wataalamu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanapata uelewa kuhusu masuala ya udhibiti ubora ikiwemo viwango na mbinu za udhibiti ubora ili kuboresha utendaji kazi, kuongeza tija na ufanisi.

Mafunzo hayo yamefunguliwa na Mkurugenzi wa Usuluhishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, George Mandepo. Mafunzo hayo yamefanyika Kibaha mkoani Pwani na kuhudhuriwa na wajumbe wa Menejimenti wa OWMS na watumishi wa Idara na Vitengo mbali mbali ambayo yatafanyika kwa muda wa siku mbili.

Mandepo amesema kuwa mafunzo hayo ni adhimu na muhimu kwa viongozi na watumishi wa OWMS kwa kuwa yataleta chachu na kuongeza mbinu za kuwahudumia wateja kwa kuzingatia viwango na ubora unaotakiwa hivyo kuendana na matakwa ya wateja, mabadiliko katika utoaji huduma na kuweza kwenda na wakati.

***"Mafunzo haya yanafanyika wakati muafaka na yanakwenda sambamba na Dira ya Ofisi hii ambayo ni kuwa Ofisi mahiri ya umma ya kuendesha kesi na mashauri ya madai yanayoihusu Serikali, hivyo mafunzo haya hayaepukiki na muhimu kwetu ili Ofisi iweze kutoa huduma bora zaidi katika kutekeleza majukumu yake,"*** amesisitiza Mandepo.

Mkufunzi wa mafunzo hayo kutoka TBS, Bi. Magdalena Sademaki amesema kuwa mafunzo hayo yataboresha utendaji kazi na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu kwa kuzingatia mifumo ya taasisi iliyowekwa, kujenga umoja, ushirikiano katika kazi, kupunguza urasimu, kutoa huduma kwa wakati kwa wateja wa taasisi, matumizi mazuri ya rasilimali na kutekeleza mipango iliyowekwa kwa uhai wa taasisi ili kufikia malengo ya Serikali.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi, Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora na Menejimenti ya Kesi, Bi. Alice Mtulo amewaomba washiriki kuwa watulivu na kusikiliza kwa makini mafunzo hayo ili kuleta tija kwa Ofisi katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali
08 Septemba, 2023



*Mkurugenzi wa Usuluhishi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, George Mandepo akifungua mafunzo ya Udhibiti Ubora kwa Menejimenti ya Ofisi hiyo yaliyofanyika Kibaha, Pwani. Kushoto kwake ni Kaimu Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora wa Ofisi hiyo, Bi. Alice Mtulo.*



*Viongozi na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa kwenye picha ya pamoja wakati wa mafunzo ya udhibiti ubora yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani. Aliyesimama mbele katikati ni Mkurugenzi wa Usuluhishi wa Ofisi hiyo, George Mandepo aliyefungua mafunzo hayo. Wa kwanza kulia ni Mkufunzi kutoka Shirika la Viwango Tanzania, Bi. Magdalena Sademaki.*

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 690<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |